HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kumb.Na.BDC/ S.10/15/81 **25/05/2022**

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA KUOMBA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:-

1. **KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III (NAFASI - 3)**
   - Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV).
   - Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu.
   - Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika 1.
   - Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka katika chuo chochote kinachotambuliwa na serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher

KAZI NA MAJUKUMU:

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
2. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
3. Kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi na ratiba ya kazi nyingine,
4. Kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

MSHAHARA:

- Ngazi ya Mshahara wa Serikali ni **TGS B** kwa mwezi.

2. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI - 2)

Kuajiriwa mwenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya daraja la B au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- Kufanya usafi wa gari, na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

MSHAHARA:

- Ngazi ya Mshahara wa Serikali ni **TGS B** kwa mwezi.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya elimu, taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha ndogo mbili za rangi (passport size).
3. Waombaji wote waambatanishe na maelezo binafsi yaliyojitosheleza (detailed C.V) yenye anwani na namba za simu.
4. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wav yeti vyao kutoka Baraza na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
5. Waombaji wote watakaokidhi sifa wataitwa kwenye usaili.
6. Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (Original Certificates).

NB: Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo;

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI
S.L.P 111,
BUMBULI.

Mwisho wa kutuma barua za maombi ni tarehe 07/06/2022 saa Tisa na Nusu Alasiri (9:30).

George D. Haule
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILA
BUMBULI